



NEW

JAMHURI YA MUUNGANO TANZANIA

SOMA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

Kumb.DCC/CF.1/10

12/12/2024

TANGAZO LA AJIRA YA MUDA

Mkurugezi wa JIJI Dar es Salaam anawatangazia Watanzania wote wenye sifa nafasi ya kazi ya kukusanya ushuru wa Soko pamoja na wafanya Usafi.

I. WAKUSANYA USHURU WA SOKO (NAFASI - 43)

SIFA ZINAZOHITAJIKA

1. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne
2. Awe na elimu ya Cheti/ Stashahada ya Uhasibu au Uongozi wa Biashara kutoka Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

KAZI/MAJUKUMU

1. Kukusanya ushuru wa Soko
2. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na msimamizi wake.

II. WAFANYA USAFI (NAFASI 41)

SIFA ZA KUAJIRIWA.

1. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne

KAZI/MAJUKUMU.

- Kufanya usafi katika Soko la Samaki Feri
- Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake.



MASHARTI KWA UJUMLA:

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
2. Awe amehitimu na kupata cheti cha kidato cha Nne
NB:"Results Slip" hazitakubadilika.
3. Awe na cheti cha kuzaliwa.
4. Awe na umri kati ya miaka 18-45.
5. Ajira ni ya mkataba wa miezi sita [6].
6. Mwajiri atalipa mshahara wa Tsh.10,000 kwa siku yenye kuleta jumla ya 300,000/= kwa mwezi.

Barua zote ziambatane na nyaraka zifuatazo:

- (i) Nakala za vyeti vya mwombaji vilivyothibitishwa ambayo ni:
 - Cheti cha kidato cha nne
 - Cheti cha Taaluma
 - Cheti cha Kuzaliwa.
 - Kitambulisho cha Taifa
- (ii) Picha ndogo ya rangi (colored Passport size moja ya hivi karibuni).
- (iii) Waombaji wenye sifa pungufu au zaidi na zilizotajwa hapo juu hawaruhusiwi kuomba kwani maombi yao hayatafanyiwa kazi.


Barua ambazo hazikuambatanishwa na nyaraka zilizotajwa hapo juu hazitashughulikiwa.

JINSI YA KUTUMA MAOMBI:

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na anwani kamili ya mwombaji pamoja na namba ya simu zitumwe kwa anuani ifuatayo hapa chini;

**MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI
S.L.P. 20950
DAR ES SALAAM.**

Mwisho kupokea maombi ni tarehe 23/12/2024 saa 9.30
Mchana. Imetolewa na:


Elihuruma S. Mabelya
MKURUGENZI WA JIJI